DISTINCTION NATIONAL EXAMINATION PANEL

JARIBIO LA PILI LA KC.P. E - 2016

DARASA LA NANE

8

002

KISWAHILI LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lolote lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   NAMBA YAKO YA MTIHANI
   JINA LAKO
   JINA LA SHULE YAKO
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu zako wewe mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ni sahihi. Chagua jibu hilo
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu

Mfano

21. Kamilisha methali: Ukiona vyaelea_____

A. vyaenda
B. vyaundwa
C. vyazima
D. vyaisha

Jibu sahihi ni B

Katika karatasi ya majibu

1. [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [C] [D] **21** [A] [B] [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilochochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa

Karatasi hii ya maswali ina kurasa 7 zilizopigwa chapa

DISTINCTION EDUCATIONAL PUBLISHERS
YOU DREAM WE FULFIL

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi

Kiongozi yeyote ___1___ kuwa mwadilifu ___2___ wale anaowaongoza watatazama na ___3___ nyendo zake. Hii ni kuambatana na methali isemayo, '___4___.' Iwapo hulka zake zitaenda ___5___ maadili, basi ___6___ ajabu kuziona tabia za aina hiyo ___7___ miongoni mwa wadogo wake. Ni vyema kujiangalia sana tusije ___8___ wengine.

1. A. ana budi B. hana budi C. haibidi D. hatabidi

2. A. ingawa B. ijapokuwa C. angalau D. madhali

3. A. kuyaiga B. kuliiga C. kuziiga D. kuviinga

4. A. Mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina
B. Akikalia kigoda mtii
C. Ukubwa ni jaa
D. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba

5. A. mbali na B. sawa na C. kando mwa D. kinyume na

6. A. itakuwa B. haitakuwa C. hayatakuwa D. hakitakuwa

7. A. yakidhihirika B. ikidhihirika C. zikijidhihirisha D. ukijidhihirisha

8. A. kuwapotosha B. kupotea C. kumpotosha D. kujipotosha

Ufugaji wa kuku ni kazi ___9___ uangalifu ___10___. Vizimba sharti viwekwe ___11___ wakati wote ___12___ kuzuia kuzuka kwa magonjwa. Magonjwa ___13___ kuku sana ni ___14___. Vifaranga huchanjwa kwa madhumuni ya kuyaepuka magonjwa. Kuku ___15___ vizuri huzaana haraka sana.

9. A. unaohitaji B. unayohitaji C. inahitaji D. inayohitaji

10. A. mingi B. kubwa C. mkubwa D. nyingi

11. A. safi B. visafi C. msafi D. pasafi

12. A. wala B. ili C. bali D. ila

13. A. inayowaua B. zinazowaua C. wanaowauwa D. yanayowauwa

14. A. kifaduro na kichocho B. kideri na mdondo
C. kupooza na chelebuni D. kifafa na kideri

15. A. wanaokulishwa B. wanayelishwa C. wanaolishwa D. inayolisha

Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa

16. Chagua sentensi iliyo na **kivumishi cha kuonyesha.**
A. Mkate huo haujapakwa siagi.
B. Duka lake limefungwa leo.
C. Makaa meusi yanafuka moshi.
D. Kiatu chenyewe kinahitaji soli

17. Andika wingi wa sentensi ifuatayo.
Ufito mrefu utatumiwa kujengea jumba lile.
A. Fito mrefu zitatumiwa kujengea majumba yale.
B. Fito ndefu zitatumiwa kujengea jumba lile
C. Fito refu zitatumiwa kujengea majumba yale
D. Fito ndefu zitatumiwa kujengea majumba yale

18. Vitu vyote vinavyotokana na maumbile k.v madini, misitu, wanyamapori, bahari n.k ambavyo hupatikana katika mazingira ni
A. maliasili B. malighafi
C. maduhuli D. mali

19. Neno **amkia** lina silabi ngapi?
A. Tatu B. Tano
C. Nne D. Mbili

20. Bainisha orodha yenye **nomino za jamii** pekee.
A. Ami, mkoi, umbu, mkazahau.
B. Fungu, kipeto, bumba, maktaba.
C. Uji, mchele, matope, mazingira.
D. Woga, wema, ushindi, uhodari.

21. Mvuvi ameketi **ukingoni mwa** bahari Maneno yaliyokolezwa ni aina ya
A. kiwakilishi
B. kitenzi
C. kiunganishi
D. kihusishi

22. Ukimkanyaga mwenzako bila kukusudia utamwambiaje?
A. Kunradhi B. Simile
C. Makiwa D. Pole

23. Mashairi ya majibizano baina ya watu wawili huitwa
A. guni B. tenzi
C. ngonjera D. tarbia

24. Chagua sentensi iliyotumia **'kwa'** kuonyesha lengo
A. Kiwete alinitazama kwa huruma.
B. Daktari alikutibu kwa vidonge
C. Tayari wamejiandaa kwa safari yao.
D. Tutaenda kwa mamamkuu kumsalimia

25. landike sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa
"Nitawajuza matokeo yenu kesho," mwalimu akatuambia.
A. Mwalimu aliwaambia kuwa angewajuza matokeo yao siku iliyofuata.
B. Mwalimu aliwaambia kuwa atawajuza matokeo yao kesho
C. Mwalimu alituambia kwamba atatujuza matokeo yetu kesho
D. Mwalimu alituambia kuwa angetujuza matokeo yetu siku iliyofuata.

26. Nchi gani **si** kisiwa?
A. Ushelisheli B. Uhabeshi
C. Unguja D. Bukini

27. S ensi gani ina **kirejeshi - O cha tamati**?
A. Mtoto achezaye pale ni wake.
B. Maji yanayochemka ni ya kuogea.
C. Jumba litakalojengwa ni la waziri
D. Mikate inayookwa haitauzwa huku

28. Tegua kitendawili
Yaenda mbali lakini haiondoki ilipo
A. Ndege B. Radi
C. Sauti D. Njia

29. Mwuzaji maji rejareja huitwaje?
A. Machinga B. Manju
C. Mzegazega D. Hamali

30. Chagua sentensi iliyo katika wakati uliopo hali isiyodhihirika
A. Mimi nala chakula
B. Mguu wa mchezaji umeteguka.
C. Kaniletee uji wa wimbi
D. Ukitenda wema utatuzwa.

Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40

Mitihani imetumiwa siku nyingi kama kigezo cha kupimia werevu wa mwanafunzi katika kutekeleza majukumu ya kiakili yenye kuhitaji stadi mbalimbali. Hii ni njia ya kuaminika na rahisi ambayo imetumiwa miaka mingi na watahini kukadiria uwezo wa mtu. Lakini wale wanaoipinga mitihani wanasema kuwa, mitihani haipimi kwa njia inayoaminika uwezo wa kiakili wa mwanafunzi; badala yake mitihani inakadiria tu uwezo wa mwanafunzi wa **kukariri mambo kama kasuku** kwa muda mfupi uliojaa vitisho na shinikizo.

Wasiothamini mitihani pia wanadai kuwa mitihani humpa mtahiniwa wasiwasi mwingi. Hii ni kwa sababu **hadhi** na umuhimu wa mtihani umekuzwa sana miongoni mwa watahiniwa na jamii nzima kwa jumla. Mtihani ndio kigezo pekee kinachokadiria kufaulu au kutofaulu kwa mwanafunzi. Mustakabali wa mwanafunzi huamuliwa na mtihani. Watahini hawajali sana masuala mengine ambayo yanaweza kuathiri jinsi mwanafunzi anavyoweza kuufanya mtihani. Kwa mfano mtahiniwa anaweza kuwa mgonjwa siku ya mtihani au pengine mvyele wake mmoja anaweza kuwa akiugua, ama labda hakulala vizuri siku iliyotangulia mtihani. Haya yote ni masuala yanayoweza kumfanya mtahiniwa kutofanya vizuri katika mtihani.

Elimu nzuri humfunza mwanafunzi kutumia akili yake. Lakini mfumo wa elimu unaopendelea mtihani haufanyi hivyo. Mfumo wa aina hiyo husisitiza kufundisha yale yanayopatikana katika mwongozo uliotolewa tu.

Mwanafunzi hapewi motisha ili **kusoma kwa mapana na marefu** ili kupanua akili yake. Badala yake mwanafunzi hufungiwa kwenye uwanja finyu ambamo haruhusiwi kutoka. Mwalimu naye kadhalika hana uhuru wa kumfundisha mwanafunzi kile anachofikiria kuwa muhimu katika maisha. Badala yake jukumu kubwa analoachiwa mwalimu huwa ni kumpa mwanafunzi mbinu za kujibu maswali na kupita mtihani.

Ingawa wanaoitetea mtihani hudai kuwa matokeo ya mtihani ni ya kuaminika kwa sababu husahihishwa na watu wasiowajua watahiniwa, lakini ni vizuri pia kukumbuka kuwa watahini ni binadamu tu. Binadamu huchoka, hubanwa na kapu na zaidi ya yote, anaweza kufanya makosa. Licha ya hayo yote watahini hutakiwa kusahihisha rundo kubwa la karatasi kwa muda mfupi

Mjadala uliopo kati ya wanaopendelea mtihani na wale wasiopendelea watukumbusha kuwa kuna haja kubwa ya kuendelea kuboresha mfumo wa mitihani ili uweze kukadiria kwa yakini uwezo wa kiakili wa mtahiniwa.

31. Lengo la mtihani ni
A. kuchuja wanaojiunga na shule za upili
B. kutathmini kazi ya mwalimu na mwanafunzi.
C. kupima uwezo wa kutumia akili
D. kuwazindua wanafunzi wazembe shuleni

32. Yeyote anayefanya mtihani ni
A. mtahiniwa
B. mtihaniwa
C. mtahini
D. mdhamini

33. **"Kukariri mambo kama kasuku"** ni fani gani ya lugha?
A. Istiara
B. Nahau
C. Majazi
D. Tashbihi

34. Wengine wanapinga mitihani kwamba
A. ni migumu sana
B. humhangaisha mwanafunzi
C. inachangia udanganyifu
D. wanaopita hawasomeshwi

35. Neno **hadhi** lina maana ya
A. heshima
B. sifa
C. ubora
D. manufaa

36. Mustakabali wa mwanafunzi hutegemea mtihani kwa kuwa
A. wanaofeli mitihani hawana maisha ya baadaye
B. mitihani humwezesha mtu kuishi vizuri baadaye
C. shughuli ya kujikimu baadaye huenda ikategemea matokeo.
D. mtu akifeli mitihani hawezi kufanikiwa maishani

37. Lengo kuu la elimu ni
A. kupita mitihani yote.
B. kujiimarisha na kustawisha jamii
C. kupata vyeti na sifa kemkem
D. kupata maarifa ya kusoma na kuandika

38. Msemo **kusoma kwa mapana na marefu** una maana ya
A. kusoma hadi mwisho.
B. kusoma na kufuzu mitihani
C. kusoma kwa lengo la kujiburudisha
D. kusoma kwa namna mbalimbali

39. Uhuru wa mwalimu hudhibitiwa na mitihani kwa kuwa
A. hapaswi kufunza lililo nje ya mwongozo
B. wanafunzi hawafuati yaliyo nje ya mwongozo
C. muda mwingi ni wa kufunza yanayotahiniwa tu
D. hana vitabu vya kuwafaa wanafunzi.

40. Mwito wa mwandishi wa makala haya ni kuwa
A. mfumo wa kutahini upigwe msasa
B. mbinu za sasa za kutahini ziko sawa
C. mfumo wa kutahini upigwe marufuku.
D. njia mbadala itafutwe badala ya mtihani

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50

Maisha ya vijijini yalimchukiza mno Bakari. Daima alilalamikia ukosefu wa vifaa vya kisasa kama vile barabara za lami, magari ya kifahari na majumba ya starehe yaliyokuwa mjini. Haikumpitikia kamwe kuwa siku moja angekinaishwa na maisha haya.

Bakari alijitoma jijini mara tu baada ya kukamilisha masomo yake ya kidato cha nne. Kama ghulamu yeyote yule wa umri wake, alikuwa na matamanio na ndoto za ajabu. Alijiona akiendesha mojawapo la magari yaliyoendeshwa na wapitanjia. Alitamani kuishi katika jumba zuri kama aliloishi mjomba wake. Laiti angalilipa wazo zito shauri la baba yake la kuliendeleza shamba lao kubwa.

Miezi ya mwanzomwanzo aliona raha kuamka asubuhi kutafuta kazi bora kuliko ya shambani. Akajiunga na wenzake kupigania vibarua ambavyo vilikuwa vimeadimika katika eneo la viwanda. Mara mojamoja aliambulia **kibarua cha sulubu** ambacho kilichakaza viganja na akili zake. Mara nyingi hakupata kibarua chochote na ilimbidi kula mate, sikwambii kustahimili kelele za mwenye nyumba kwa kuchelewa kulipa pango. Bakari akaanza kuhofia na kutilia shaka ufanisi aliotarajia kupata.

Siku zilivyosonga ndivyo hali ya kukata tamaa ilivyomzonga. Maisha ya mji yalijaa vurumai na zogo za kila nui. Kelele za wapiga maji, miziki ya kupasua viwambo vya masikio, mioshi kutoka kwenye viwanda na magari makuukuu, kelele za wachuuzi mitaani na mengine mengi. Haya yote hakuwa ameyatarajia. Hakuwa ametarajia kwamba ingembidi kutembea akishikilia mifuko yake ya shati na suruali asije akapoteza riziki yake ya pekee ya siku hiyo. Kwa kweli haya siyo aliyotazamia Bakari.

"Itabidi nitafute jingine la kuegemea. Kule mashambani kulikuwa afadhali. Kuna usalama, udugu, hewa safi na mengine mengi ya kutamaniwa." Akajisemea huku akifunganya virago kurudi mashambani kushika tope.

41. Maisha ya kijijini yalimchukiza Bakari kutokana na
A. majengo na magari ya kifahari mjini.
B. upungufu wa ustaarabu wa kisasa.
C. adha na usumbufu wa wazazi wake
D. ukosefu wa shughuli zozote za kufanya.

42. Aya ya kwanza inatudokezea kuwa,
A. Bakari angekosa hamu ya maisha ya mji baadaye
B. Bakari aliwahi kuishi mjini hapo awali
C. Bakari alipata raha ya mjini kikamilifu
D. Bakari alibadili nia ya kuenda mjini.

43. Ilikuwa vigumu kwa Bakari kupata kazi kutokana na
A. umri wake mdogo.
B. ukosefu wa elimu.
C. elimu duni na nafasi haba.
D. kutoelewa mji vizuri

44. Bakari alijiona akiishi katika jumba zuri na kuendesha gari la kifahari. Ama kweli, _____
A. alikuwa juu juu kama ninga
B. aliota kama Alinacha
C. aliwaka kama moto wa kifuu
D. alichanua kama waridi

45. **Kibarua cha sulubu** alichoambulia Bakari ni
A. kazi ngumu ya muda mfupi.
B. kazi ya muda ya kipato haba.
C. kazi ya lazima ya mapato duni
D. kazi ya lazima ya muda mfupi

46. Bakari alipokosa kazi
A. alilala njaa
B. aliomba msaada
C. aliamua kuiba
D. alilala nje

47. Ipi si miongoni mwa kero za mji?
A. Uporaji wa mali
B. Muziki wenye sauti kubwa.
C. Udugu na utagamano
D. Zogo la wachuuzi

48. **"Itabidi nitafute jingine la kuegemea. Kule mashambani kulikuwa afadhali."** Maneno haya yanaonyesha kuwa Bakari
A. anajutia uamuzi wake wa sasa
B. hajaliona lolote zuri katika mji
C. amekerwa na kelele za mwenye nyumba.
D. anajutia uamuzi aliofanya awali

49. Kero la wapiga maji lilikuwa
A. kulewa sana
B. kelele zao
C. lugha duni
D. kupiga milango

50. Kichwa kifaacho zaidi kwa makala haya ni
A. Kiingiacho mjini si haramu.
B. Baada ya dhiki faraja.
C. Mchuma janga hula na wa kwao
D. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani